JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



# Mwelekeo wa Rais Samia Suluhu Hassan katika Kutetea na Kuimarisha Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania

Septemba 2022

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
TANZANIA
COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS AND GOOD GOVERNANCE

***"Haki za binadamu...zimetambuliwa kwenye Katiba yetu...tumesaini na kuridhia mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za binadamu...tumeanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hapa nchini, ambapo moja ya majukumu yake ni kupokea malalamiko na kufanyia uchunguzi...Pia nchi yetu inaongozwa na sheria na hakuna aliye juu ya sheria."***

***- Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.***

# 1.0 UTANGULIZI

Kijitabu hiki kinatoa taarifa ya tathmini ya mchango wa Rais wa Awamu ya Sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan katika kukuza, kulinda na kutetea haki za binadamu nchini. Pia, kinaweka kumbukumbu ya mambo mengi aliyoyafanya katika sekta ya haki za binadamu na utawala bora kuanzia Machi 2021 hadi Septemba 2022.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo ni taasisi ya kitaifa yenye dhima ya ukuzaji na ulinzi wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini inaungana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kutambua mchango wa Mheshimiwa Rais wa kutetea na kulinda haki za binadamu nchini.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, watetezi wa haki za binadamu, viongozi na watumishi wa

umma na sekta binafsi, na mwananchi mmoja mmoja tunaunga mkono kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Rais na Serikali yake. Tunalo deni la kulipa, nalo ni kufuata nyayo zake kwa ustawi wa Taifa letu.

# 2.0 JITIHADA ZA MHESHIMIWA RAIS SAMIA KATIKA KUIMARISHA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA NCHINI

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani ameonesha utashi mkubwa wa kisiasa kuhusu kulinda, kukuza, na kuendeleza hifadhi ya haki za binadamu na uzingatiaji wa misingi ya utawala bora nchini. Hii inadhihirishwa kupitia hotuba na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa chini ya uongozi wake. Katika kipindi cha uongozi wake kila mara matamshi yake yamekuwa yakigusa haki za binadamu na misingi ya utawala bora na hivyo anastahili pongezi nyingi.

Azma ya Mheshimiwa Rais katika kulinda, kukuza na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora inaweza kuthibitishwa katika maeneo mengi. Miongoni mwa maeneo hayo ni pamoja na yafuatayo:

## 2.1 Uhuru wa habari na vyombo vya habari

Baada ya kuingia madarakani amevielekeza vyombo vya habari kutekeleza majukumu yake kwa uhuru. Hatua hii imeuwezesha umma kupata habari mbalimbali bila kikwazo chochote. Aidha, vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa na Serikali kama vile gazeti la Tanzania Daima, Mwanahalisi, Mawio pamoja na Televisheni mtandao vilifunguliwa ili kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhabarisha umma na

kupanua wigo kwa wananchi kufurahia haki yao ya kikatiba ya kupata habari.

Hivi sasa iwapo itatokea habari imechapishwa kinyume na sheria za nchi atakayewajibika ni mwandishi wa habari na siyo chombo cha habari. Pia, Mheshimiwa Rais ameruhusu wananchi, ikiwemo vyombo vya habari kumkosoa yeye pamoja na Serikali yake, lakini ametaka ukosoaji huo ufanywe kwa staha.

Kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya habari anaendelea kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Rais. Akizungumza kupitia kituo cha televisheni cha ITV kwenye kipindi cha dakika 45, Mheshimiwa Nape Nnauye, alisisitiza kauli ya Mheshimiwa Rais kwa kusema:

***"…tuikosoe Serikali kadri tunavyoweza isipokuwa tuikosoe kwa staha, tusikosoe kwa kudhalilisha, unataka kumsema Nape kakosea mseme kwa heshima, usisahau kwamba na yeye ni binadamu."***

Ni wazi kuwa hatua hizi zinawapa fursa waandishi wa habari kutekeleza majukumu ya kuhabarisha umma na kufichua maovu bila woga, ambapo ni hatua bora kwa ustawi na maendeleo ya taifa, kwa mujibu wa Mheshimiwa Rais.

## 2.2 Haki ya kupata habari

Uwepo wa vyombo huru vya habari unapelekea wananchi kupata habari mbalimbali kupitia vyombo hivyo. Hatua hii inaenda sambamba na upatikanaji wa habari kwa wananchi bila malipo. Vyombo vya habari vya ndani (local media) hasa televisheni na radio vinapatikana bure ili mradi mwananchi awe na televisheni na king'amuzi.

Huduma za mitandao ya kijamii na televisheni mtandao zinapatikana kwa gharama nafuu. Vile vile, vyombo vya habari vya ndani kama vile televisheni za ITV, TBC1, Clouds, Channel Ten, Star TV zinapatikana kwenye ving'amuzi vyote bila gharama yoyote. Kufuatia hatua hii, matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora yamekuwa yakitolewa taarifa mara yanapotokea na hivyo mamlaka husika za Serikali ikiwemo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuchukua hatua kwa wakati na kwa mujibu wa sheria.

## 2.3 Haki ya kuishi na usalama wa raia

Matukio ya wananchi kujichukulia sheria mkononi na kuua raia wenzao kwa tuhuma mbalimbali yamepungua. Akinukuliwa na Gazeti la Habari Leo la Septemba 4, 2021 aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai, Kamishna wa Polisi Camillius Wambura alieleza kuwa kwa mwaka 2021/2022 watu zaidi ya 300 waliuawa na wananchi kwa kujichukuliwa

sheria mkononi, ambapo watu 239 waliuawa kwa tuhuma za wizi na mifugo kula mazao shambani, na watu 84 waliuawa kwa tuhuma za ushirikina.

Mhe. Rais, katika hotuba yake aliyoitoa Julai 20, 2022 jijini Dodoma wakati wa hafla ya uapisho wa viongozi mbalimbali alilitaka Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa ufanisi na kuimarisha usalama wa raia na mali zao na kuzingatia haki za binadamu.

Pia, katika hotuba yake wakati wa uzinduzi wa kamati ya kitaifa ya ushauri kuhusu utekelezaji wa mpango kazi wa ahadi za nchi kwenye Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa Desemba 16, 2021 jijini Dodoma alilitaka Jeshi hilo kuhakikisha linatenda haki na linasogeza huduma zake karibu zaidi na wananchi hususan katika maeneo ambako hazipo. Katika hafla hiyo alisema maneno yafuatayo:

*"Lakini inawezekana pia kesi haziji vituoni kwa sababu watu wamekata tamaa, pengine ukienda kwenye jamii ndani huko kuna makesi chungumzima ambazo polisi mngeyashughulikia lakini haziji kwa sababu watu wamekata tamaa; pengine wakija hawapati haki zao lakini inawezekana pia sababu maeneo mengine vituo vya polisi vipo mbali kwa hiyo mtu asafiri kwenda huko kupeleka kesi anaona tumalizane huku huku kivyetuvyetu hiyo ndiyo inayoleta watu kuchukua sheria mkononi. Kwa hiyo pamoja na sifa kwamba tumepunguza makosa lakini*

*tuangalie factors nyingine zinazofanya makosa yapungue au tusiwe nayo; inawezekana kuna makosa ambayo hatukuyapata, lengo langu hapa kusema Jeshi la Polisi lisambae zaidi huko kwenye jamii na kwenda kuweka usalama kwa watu lakini kuzuia watu kutochukua sheria mkononi kwao."*

Katika kipindi hicho, kumekuwa na matukio yaliyotolewa taarifa na vyombo vya habari kuhusu mauaji ambapo Jeshi la Polisi lilituhumiwa kuyatekeleza na hivyo kuvunja haki ya kuishi kwa raia. Mheshimiwa Rais amekuwa akivikemea vikali vitendo hivyo. Akifungua kikao kazi cha Maafisa Wakuu wa Jeshi la Polisi Makao Makuu, na Makamanda wa mikoa na vikosi vya Jeshi la Polisi Agosti 25, 2021 Mheshimiwa Rais alisema:

*"Lakini kwa pamoja niliyoyasema Jeshi la Polisi ndugu zangu baadhi yenu mnashutumiwa kwa kutofanya haki kwa jamii kwa hiyo naomba muangalie kwa vile vitendo mnavyofanya...Tuko hapa kuhudumia watu siyo kudidimiza watu. Nadhani matumizi makubwa ya nguvu IGP muyatazame, kesi za kufa watu kwenye vituo vya polisi hazileti sifa nzuri kwa Serikali, naomba sana ndugu zangu tendeni yaliyo haki."*

Kwa ujumla Mheshimiwa Rais amekuwa akiwaelekeza wasaidizi wake katika ngazi zote kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora bila kumwonea mtu yeyote. Ni wajibu wa

Serikali ikiwemo Tume na wadau wengine kukemea matukio hayo na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika.

## 2.4 Haki ya kuwa huru

Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza uhuru kwa wananchi wote katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya sheria. Amekemea ukamataji wa raia usiozingatia sheria na taratibu; raia kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria; watuhumiwa kunyimwa dhamana kwa kesi zenye dhamana; raia kubambikizwa kesi; ucheleweshaji wa kuanza kusikilizwa kesi kwa kisingizio cha kukamilisha upelelezi; na usafirishaji haramu wa binadamu. Mheshimiwa Rais amedhihirisha hili kwa vitendo ambapo watuhumiwa wengi wa kesi mbalimbali wameachiwa huru. Katika hotuba yake ya Agosti 25, 2021 ya kufungua kikao kazi cha Maafisa Wakuu wa makao makuu, na Makamanda wa mikoa na vikosi vya Jeshi la Polisi Mheshimiwa Rais alisema:

*"Nitoe wito mara mbili, mara moja kwa zile kesi ambazo mnahakika upelelezi hautakamilika, hao watu watolewe wakafaidi uhuru wao wakiwa nje, kama kesi haina muelekeo na hili nalisema kwa mara ya pili sijui mara ya tatu basi hawa watu watolewe, lakini kwa zile kesi ambazo mnauhakika upepelezi utatimia basi uharakishwe kama mlivyojiwekea muda hapa miezi sita mpaka mwaka."*

Pia alisema: *"Lakini kwa upande mwingine mwanadamu ni mwanadamu na ana uhuru wake,*

*naomba mkae na wadau wengine muangalie uwezekano wa kurekebisha sheria ya kuweka mtu mahabusu. Haki kwa jamii ndiyo wajibu wetu mkubwa."*

## 2.5 Haki za kisiasa

Katika eneo hili yaliyofanywa na Rais wa Awamu ya Sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan siyo haba.

i) Ameruhusu vyama vyote kushiriki siasa kwa misingi ya kidemokrasia na haki kwa kuzingatia siasa za kistaarabu;

ii) Ameruhusu wananchi, wanasiasa, wanaharakati na viongozi wengine kukosoa utendaji wa Serikali yake na yeye binafsi kistaarabu;

iii) Amemwelekeza Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kufuta kesi zinazodaiwa kuwa na mwelekeo wa kisiasa ambapo Mkurugenzi aliyafanyia kazi maelekezo hayo kwa kuzifuta kesi hizo. Kwa mfano, Machi 10, 2022 aliifuta kesi ya Jinai Na. 467/2022 iliyokuwa ikiwakabili wanachama 36 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) jimbo la Buyungu mkoani Kigoma. Aidha, Februari 27, 2022 wanachama 36 wa chama hicho waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya ugaidi huko Mkoani Mwanza walifutiwa kesi. Pia, Machi 2022 Mwenyekiti wa CHADEMA nchini,

Mheshimiwa Freeman Mbowe na wenzake watatu (3) walifutiwa kesi ya ugaidi. Hatua hizi zinalenga kuweka mazingira sawa kwa vyama vyote vya siasa nchini.

Hatua zilizochukuliwa na Rais kuhakikisha kunakuwepo na usawa kwa vyama vyote vya siasa pamoja na kuzipatia ufumbuzi kero mbalimbali za vyama vya upinzani zimewezesha vyama vya NCCR Mageuzi na CHADEMA vilivyokuwa vimesusia mikutano ya Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kufanya maridhiano na kutangaza kushiriki mikutano na mazungumzo hayo.

## 2.6 Haki za kiuchumi

Tangu iingie madarakani Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimia Rais Samia Suluhu Hassan imekuwa ikijishughulisha kwa kiwango cha hali ya juu katika kuboresha hali ya kiuchumi ya Taifa, makundi mbalimbali katika jamii na mtu mmoja mmoja na imetambua nafasi ya sekta binafsi katika ukuzaji wa uchumi. Kwa ufupi hatua mbalimbali zimechukuliwa na kuonesha kuzaa matunda.

*"Serikali itashirikiana kuikuza na kuendeleza sekta binafsi ndiyo lengo letu katika mpango huu na katika sekta binafsi kundi lenu ni sekta binafsi na katika maeneo kadhaa nilikuwa naongea kwamba lengo letu ni kuwafanya Wamachinga wakae mahali pazuri, wafanye biashara vizuri, wahitimu watoke kwenye*

*machinga waingie kundi maalum la wafanyabiashara ili tutanue wigo wa kulipa kodi, kwa hiyo lengo letu Serikali ni hilo...Na kutokana na lengo hilo yale yote ambayo mmeyasema kama changamoto tunayaelewa na tunaenda kufanyia kazi."*

Mheshimiwa Rais alisema hayo katika hotuba yake wakati wa mkutano wake na Wafanyabiashara wadogo wadogo, maarufu Wamachinga Januari 25, 2022 jijini Dar es Salaam.

Aidha, katika kuyapa uzito masuala ya kiuchumi nchini, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan iliunda Kamati ya Ushauri ya kitaifa kuhusu utekelezaji wa mpango kazi wa ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa; Na wakati wa uzinduzi wa Kamati hiyo Desemba 16, 2021 jijini Dodoma Mheshimiwa Rais alisema:

*"Kamati hii ni chombo muhimu cha kusimamia na kushauri namna bora ya kuhakikisha ahadi za kuinua haki za uchumi kwa jamii yetu hasa wanawake zinatekelezwa vyema na malengo yake yanafikiwa."*

## 2.7 Haki za huduma za kijamii

### *2.7.1 Haki ya elimu*

Katika kuhakikisha watoto wote wananufaika na elimu, Mheshimiwa Rais ameendelea kutoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari. Aidha, Novemba 24, 2021 Serikali yake ilitoa tamko la

kuruhusu kurejeshwa shuleni wanafunzi waliokatiza masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali; ikiwemo utoro, utovu wa nidhamu, na kupata ujauzito. Hata wale waliofeli shule ya msingi sasa wanayo fursa ya kurejea katika mfumo rasmi wa elimu na kuendelea na masomo yao kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

*"Tumeamua kuwa watoto wote walioacha Shule kwa sababu mbalimbali - utoro, sababu za kisheria, kwamba ukipata mimba huruhusiwi kuendelea na masomo, waliodondoka la saba, tunajua kuna wanafunzi wetu wazuri sana kwa bahati mbaya wakati wa kufanya mtihani hawakufanya vizuri lakini baada ya kukaa nje wamejutia tunawapa nafasi nyingine ya kurudi kufanya mtihani, lengo la maamuzi haya ni kutoa fursa pana kwa watoto wa kitanzania kuweza kuendelea na elimu."*

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan alisema hayo katika hotuba yake wakati wa ufunguzi wa Shule ya Msingi Museveni mjini Chato Novemba 29, 2021.

Hatua hii ni ya kupongezwa kwa sababu inazingatia matakwa ya kisheria ya kimataifa kwa Serikali zote kutoa elimu kwa watoto wote bila ya ubaguzi wowote. Pia, inaiondoa Tanzania kutoka katika kundi la mataifa machache wanachama wa Umoja wa Afrika (AU) zinazoendelea kuwatenga wasichana wajawazito kupata elimu.

Uamuzi huu pia ni hatua nzuri ya utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii wa Bara la Afrika (Ajenda 2063) unaodhamiria kujenga mtaji wa rasilimali watu kupitia uwekezaji endelevu katika elimu.

Vilevile ni utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) yanayolenga kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma katika maendeleo na kuhakikisha elimu jumuishi na bora kwa wote.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mheshimiwa Rais ametoa jumla ya Shilingi Bilioni 101.877 kwa mchanganuo ufuataao: ujenzi wa vyumba vya madarasa (Bilioni 64.38); ujenzi wa mabweni (Bilioni 8.96); ujenzi wa matundu ya vyoo (Bilioni 5.85), ujenzi ya nyumba za walimu (Bilioni 1.55); ujenzi wa maabara (Milioni 550); ujenzi wa mabwalo (milioni 600); majengo ya utawala (milioni 200); ukarabati wa shule kongwe (Bilioni 2.53); na ujenzi wa shule mpya (Bilioni 17.25). Fedha hizi zimetumika kwa ajili ya shule za msingi na sekondari kwa kila Halmashauri nchini. Aidha, ametoa wito kwa wazazi kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa na kuwa elimu ya msingi na sekondari itaendelea kutolewa bure. Jitihada hizi zimeenda sambamba na kuajiri walimu wapya kuwezesha upatikanaji wa elimu bora.

Kwa upande wa elimu ya juu, kupitia Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU), Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka Shilingi Bilioni 464 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia Shilingi Bilioni 570 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 22.8. Ongezeko hilo la bajeti lilienda sambamba na ongezeko la wanafunzi walionufaika na mikopo hiyo ambapo mwaka 2020/2021 wanafunzi 55,442 walipata mikopo huku mwaka wa fedha 2021/2022 idadi ya wanafunzi hao iliongezeka kufikia 70,000 sawa na ongezeko la asilimia 26.2, na hivyo watanzania kunufaika na haki ya elimu.

### 2.7.2 *Haki ya afya*

Sekta ya afya inalinda na kuhifadhi haki za binadamu kwa kuhudumia wananchi na hivyo kuwaepusha na kupunguza vifo kutokana na kuboreshwa kwa huduma hizo. Kwa mujibu ya taarifa iliyotolewa na gazeti la Habari Leo la Machi 4, 2022 Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu alinukuliwa akieleza kuwa, kwa mwaka 2021/2022 Serikali ya awamu ya sita ilitoa jumla ya Shilingi Bilioni 891.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, ununuzi wa vifaa tiba na dawa kwa kila zahanati, kituo cha afya, hospitali za wilaya na za rufaa ngazi ya mikoa, hospitali za Kanda na hospitali ya Taifa Muhimbili.

### 2.7.3 Haki ya maji safi na salama

"Maji ni uhai" na ni moja ya mahitaji muhimu kwa uhai wa binadamu. Katika kutekeleza haki hii, Rais Samia ametoa zaidi ya Bilioni 934.3 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji mijini na vijijini. Akizungumza na wanahabari Machi 7, 2022, Waziri mwenye dhamana ya masuala ya maji, Mhe. Jumaa Aweso alisema Wizara yake ina malengo ya kuimarisha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa zaidi ya asilimia 95 katika maeneo ya mijini ifikapo 2025 na kwa vijijini kwa zaidi ya asilimia 85. Takwimu za Wizara ya Maji zinaonyesha kuwa upatikanaji wa maji umefikia asilimia 72.3 kwa vijijini na asilimia 86 kwa mijini sambamba na kukamilika kwa miradi 1,015 ya maji ambapo 915 ni ya vijijini na 100 ya mijini.

Kwa kifupi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa kipaumbele kwenye upatikanaji wa haki ya huduma za jamii – elimu, afya na maji safi na salama, hususan kwa wananchi wa ngazi za chini; na hili linadhihirishwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali yake kama ilivyoelezwa hapo juu na kwa kauli zake pia.

Wakati akipokea taarifa ya awali ya utekelezaji wa fedha za UVIKO-19, Januari 4, 2022 Ikulu jijini Dar es Salaam, Mheshimiwa Rais alisema:

> *"Moja katika jambo linalogusa mwananchi moja kwa moja ni elimu ambapo tumeweka fedha ya*

*kutosha; cha kwanza ni elimu, la pili ni afya, afya ya mwananchi ndiyo kipaumbele chetu na huko tumekwenda na tunakwenda kwa kiasi kikubwa, lakini jingine maji ndiyo muhimu kabisa, maji tutaendelea ku-invest kuleta maji, kwa wananchi ni sekta ambazo lazima tuzifanyie kazi."*

Mheshimiwa Rais aliongeza kuwa:

*"Fedha zote hizi zilielekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele vinavyogusa wananchi moja kwa moja ili kuwaondolea kero katika kuzifikia na kuzipata huduma za afya, elimu ya msingi na sekondari na uwezeshaji wananchi kiuchumi."*

Aidha, katika hotuba yake hiyo alieleza kuwa:

*"Tunakwenda kuhakikisha mambo yanayomuhusu mtanzania kule chini ndiyo tunakwenda kuyafanyia kazi pamoja na haya ya juu huku tutakwenda ngazi ya juu lakini muhimu zaidi ngazi ya chini."*

## 2.8 Haki za wafanyakazi

Katika eneo hili Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na Serikali yake wameonesha nia ya dhati ya kuimarisha haki za wafanyakazi nchini na mambo mengi yamefanyika, ikiwemo kuwapandisha vyeo watumishi waliokaa katika cheo kimoja muda mrefu na kuwalipa stahiki zao; kuongeza mishahara; kuwalipa mafao yao watumishi wa umma walioondolewa kutokana na vyeti feki na waliokuwa na elimu ya darasa la saba, kutaja

kwa uchache.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei 1, 2021 Mheshimiwa Rais aliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kufanya tathimini ya kiasi kitakachotumika kuwalipa watumishi wa umma walioondolewa kazini kwa vyeti feki kama mafao yao.

*"Nimepokea malalamiko ya darasa la saba ambao waliondoshwa pamoja na mkumbo wa vyeti feki... Baada ya kikao changu na TUCTA na Mawaziri wanaohusika tulikaa tena kikao cha Serikali peke yetu na tuliwaza kwamba wale wote waliofukuzwa, walifanyakazi kwa muda mrefu na kwamba hawakupata chochote cha kuondoka nacho... nimewaagiza wizara pamoja na Wizara ya Fedha waangalie ni kiasi gani wafanyakazi wale walikatwa kwenye jasho la mishahara yao. Kile walichochangia kwenye mifuko walipwe. Ni ile asilimia 5 waliyokatwa kwenye mishahara yao na si ile asilimia 10 aliyokatwa mwajiri," Mheshimiwa Rais alisema.*

Aidha, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akitoa maelekezo mengi kuhakikisha kuwa wafanyakazi nchini wanapata haki zao kwa wakati na kwa mujibu wa sheria.

Kwa mfano, wakati wa uzinduzi wa Kamati ya Ushauri ya kitaifa kuhusu utekelezaji wa mpango kazi wa

ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa Desemba 16, 2021 jijini Dodoma alisema:

> *"Pamoja nalo nilihimize Jeshi la Polisi, ingawa Inspekta Jenerali amelisema vizuri kwamba wanaotoka hawa naomba watoke na kibindo cha stahiki zao tusizalishe tena madeni ya wastaafu, Serikali ikabakia na mlolongo wa madeni ya wastaafu. Kwa hiyo kazi ifanywe kila anayetoka ajue mafao anapata wapi, stahiki zake za kumhamisha, nauli zake na kufika kule anakokwenda, wawe wameondoka wakiwa wamekamilika."*

## 2.9 Haki za makundi maalumu

### *2.9.1 Haki za wanawake*

Haki za makundi maalumu zinajumuisha makundi yale yenye mahitaji maalumu kutokana na hali yao. Makundi hayo ni pamoja na: Wanawake, watu wenye ulemavu, watoto, wazee na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita haki za makundi haya zimepewa kipaumbele kikubwa; maelekezo na miongozo mbalimbali imetolewa na hatua nyingi zimechukuliwa ili kuhakikisha makundi haya yanafurahia haki zao kwa mujibu wa sheria na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imetia saini. Kuna mifano mingi ya ahadi na maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais Samia ameyatoa katika eneo hili yanayoonesha azma yake ya kuboresha haki za wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii; na ifuatayo ni baadhi yake.

Akilihutubia Taifa wakati wa maadhimisho ya siku ya demokrasia nchini Septemba 15, 2022 Mheshimiwa Rais alisema:

*"Ndugu zangu nilikuwa na nia thabiti ya kulea majukwaa yaendelee, kama mnavyojua katika kila positive kuna negative lilitazamwa kwa jicho siyo ndiyo maana likalegalega niahidi kwamba najipanga kuyalea majukwaa, kwa mwaka huu tayari nilikuta bajeti imeanzishwa kwa hiyo nisingeweza kupenyeza hiyo ajenda lakini kwa bajeti ya mwakani majukwaa yale ambayo bado yame-survive na nina taarifa ya majukwaa katika mikoa 18 yako hai naomba hayo majukwaa yajipange na wale ambao hawana majukwaa wayarudishe ili twende na safari ya maendeleo kwa wanawake."*

Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan aliongeza kuwa:

*"Ni vigumu kuzungumzia demokrasia bila kugusia masuala ya haki za wanawake na usawa wa jinsia, kama nilivyosema awali demokrasia inahusiana moja kwa moja na masuala ya haki au kwa karibu na masuala ya haki na sote tunafahamu kuwa kwenye nchi nyingi duniani, ikiwemo Tanzania wanawake kwamba ni wengi wameachwa nyuma na hii ni dosari. Lakini kwa Tanzania sasa hivi hatuzungumzii hili la wanawake kuachwa nyuma tunalozungumzia na kufanyia kazi ni changamoto zilizopo ili wanawake tuiingie pamoja na wengine kwenye mchakato wa maendeleo.*

*Kwa sisi Tanzania, kubwa ni kushikana na kufanyia kazi changamoto zilizopo natuendelee na safari yetu ya maendeleo."*

Katika maadhimisho hayo pia alisema kuwa:

*"Kwa msingi huo tunapoadhimisha siku ya kimataifa ya demokrasia hatuna budi kutafakari haki za wanawake na usawa wa jinsia na katika hilo nitumie fursa hii kuahidi kuwa Serikali itajitahidi kushughulikia masuala ya haki za wanawake na usawa wa kijinsia ili kukuza demokrasia nchini, ikiwemo kutekeleza yaliyomo kwenye mpango wa tatu wa miaka mitano wa taifa wa masuala ya haki za wanawake yaliyomo kwenye azimio la Beigin na bila kusahau malengo endelevu kuhusu wanawake."*

Kwa mujibu wa Mheshimiwa Rais katika uchumi wa wanawake Tanzania imepiga hatua kubwa sana, na hili linadhihirishwa na uwepo hapa nchini wa idadi kubwa ya wanawake wajasiriamali, wafanyabiashara wakubwa, na makontrakta. Ijapokuwa bado kuna changamoto ndogo ndogo zinazowakabili, Mheshimiwa Rais ameahidi kuzipatia ufumbuzi kuwawezesha wanawake kufanya kazi zao vizuri.

### 2.9.2 Haki za watu wenye ulemavu

Haki hii pia haikuachwa nyuma na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Serikali yake, mengi yamefanyika na yanaendelea kufanyika katika kuhakikisha kwamba

kundi hili pia linafurahia haki zao kwa mujibu wa Katiba, sheria na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa mkutano wa viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu Machi 16, 2022 Mheshimiwa Rais alisema:

*"Sote tunatambua kwamba kundi hili lina changamoto na mahitaji mahususi ambayo yanatulazimu sisi Serikali na jamii kwa ujumla kuweka mipango na mikakati mahususi kwa ajili ya kuyakidhi mahitaji hayo."*

## 2.10 Usawa wa kijinsia

*"Naziagiza Sekta zote kupitia Wizara, Taasisi, Mashirika, Wakala na Halmashauri kulipa kipaumbele swala la utekelezaji wa ahadi tulizoziweka kwenye utekelezaji wa jukwaa la usawa wa kijinsia na kuweka mikakati na bajeti ya utekelezaji wa ahadi hizi."*

– Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Rais alitoa agizo hilo Desemba 16, 2021 jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa kamati ya kitaifa ya ushauri kuhusu utekelezaji wa mpango kazi wa ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa.

Mheshimiwa Rais ameielekeza Serikali kuhakikisha kuwa unyanyasaji kwa wanawake unakomeshwa

katika ngazi zote. Ameeleza kuwa wanawake wanapaswa kutazamwa na jamii kama viumbe imara, wanaojitambua na siyo dhaifu. Mheshimiwa Rais ametekeleza hili kwa vitendo ambapo katika teuzi zake katika ngazi mbalimbali za utumishi wa umma zimewahusisha wanawake. Kwa mfano alimteua Dkt. Stergomena Lawrance Tax kuwa Waziri wa Ulinzi wa kwanza mwanamke.

Aidha, amewateua wanawake kwenye nafasi nyingine kubwa serikalini kama vile Mawaziri wa Wizara mbalimbali, Majaji wa Mahakama Kuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Wilaya, Watendaji wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wenyeviti, Wajumbe wa Bodi na Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania nchi mbalimbali.

Kuhusu usawa wa kiuchumi Rais ameelekeza kuendelea kutolewa mikopo ya wanawake kwa kila Halmashauri kwa kutenga asilimia 2 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuwakopesha wanawake kwenye vikundi vyao. Pia, ameelekeza Serikali kuweka mitaji kwa kila Mkoa itakayomwezesha mwanamke kukopa bila riba ili kufanya shughuli zao za kujikwamua kiuchumi.

## 2.11 Mfumo wa utoaji haki

Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza usawa mbele ya sheria na kila mara amewataka watendaji kutekeleza

majukumu yao bila kumwonea yeyote kwa kuwa "binadamu wote ni sawa".

Katika kuhakikisha kuwa utoaji haki unazingatia weledi na wananchi wanakuwa na uelewa, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeimarisha mfumo wa utoaji haki nchini kwa kuanza kutumia lugha ya Kiswahili katika uandishi wa sheria na shughuli za utoaji haki mahakamani sambamba na kuimarisha mfumo wa utatuzi wa migogoro nje ya mahakama kwa kutumia njia ya majadiliano, upatanishi na usuluhishi.

Akizungumza na wanahabari, aliyekuwa Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa George Simbachawene Machi 11, 2022 alieleza kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja madarakani Rais Samia alihakikisha uwepo wa raslimali watu katika mahakama zote ambapo aliteua Majaji tisa (9) wa Mahakama ya Rufani, Majaji 21 wa Mahakama Kuu na Mahakimu 245 waliajiriwa. Aidha, huduma za kimahakama ziliboreshwa na kuimarika kwa kukamilisha ujenzi wa majengo na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya mahakama pamoja na matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa utoaji haki hivyo kupunguza mlundikano wa mahabusu na kuongezeka kwa kiwango cha usikilizwaji wa mashauri katika mahakama.

Katika wigo wa uwakilishi, Mheshimiwa Simbachawene alisema kuwa kupitia mabadiliko ya sheria, wigo wa

uwakilishi katika mfumo wa utoaji haki umeongezeka baada ya mawakili kuanza kutoa huduma ya uwakili katika Mahakama za Mwanzo pamoja na kuanzishwa kwa vituo jumuishi vya utoaji haki vya Mahakama katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Morogoro na Dodoma ili kuhakikisha utawala wa sheria na utoaji haki vinakuwepo na vinazingatiwa.

Mara nyingi Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akiwaasa watendaji wa mahakama kuwa waadilifu na kutenda haki. Katika hotuba yake aliyoitoa katika viwanja vya Chinangali jijini Dodoma wakati wa maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Sheria nchini Februari 2, 2022 alisema:

*"Sote tunafahamu jukumu la msingi la Mahakama kwa mujibu ya Ibara ya 107(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kutoa haki katika utekelezaji wa jukumu hili, Mahakama inapaswa kuzingatia sheria ili kutenda haki kwa wote bila kujali hali ya mtu kijamii au kiuchumi."*

Pia, aliongeza kuwa:

*"Niendelee kusisitiza watendaji wa Mahakama wenye dhima ya kuamua haki kuendelea kufanya hivyo bila kufungwa sana na masharti ya kiufundi, na hapa masharti ya kiufundi nina maana gani, kwamba Mwananchi anapoleta kesi yake mahakamani hajui chochote, hajui apite njia gani, anategemea Wakili kwa yule mwenye uwezo wa kuweka Wakili lakini*

*asiye na uwezo wa kuweka Wakili tunasema Serikali tunawajibu kwa kumpa wakili, lakini sidhani kama wote wanapata Mawikili lakini anayeshtakiwa ana uwezo wa kuweka Wakili, Mawakili hawa hutumia njia zao za kiufundi jinsi ya kukwepa vipengele na kuweza kumuweka hatiani au kumnyima haki mwenye haki kwa hiyo pamoja na kutumia vifungu vya sheria na ufundi mahakamani, kubwa kwa wewe unayetoa haki ni kuisikiliza nafsi yako je hapa natenda haki au sitendi haki."*

## 2.12 Mfumo wa haki jinai

Mara baada ya kuingia madarakani Rais Samia alitaka wananchi kutendewa haki na vyombo vya utoaji haki. Alikemea tabia ya wananchi kubambikwa kesi kunakopelekea uwepo wa idadi kubwa ya mahabusu katika magereza mbalimbali nchini, na alitoa maelekezo kwa taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:

**i)** Mheshimiwa Rais aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufuta kesi zote ambazo ushahidi wake haujitoshelezi. Agizo hilo limetekelezwa na kesi 147 za kubambikizwa zimefutwa mara moja na TAKUKURU. Aidha, Mheshimiwa Rais ametoa msamaha kwa baadhi ya mahabusu kama vile Mashehe wa uamsho na kesi nyingine Jamhuri iliamua kutoendelea nazo na hivyo mahabusu kuachiwa huru; Mfano kesi ya Mfanyabiashara na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya kufua

umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), Bwana James Rugemarila kufutiwa mashtaka ya kesi ya uhujumu uchumi baada ya kukaa mahabusu kwa miaka minne.

ii) Kuhusu Jeshi la Polisi, Rais katika hotuba zake amekemea waziwazi ubambikizaji wa kesi, wananchi kufia mikononi mwa polisi, ulemavu unaosababishwa na vipigo vya polisi. Ametaka dhamana zitolewe kwa kesi zenye haki ya dhamana bila masharti. Wakati akizindua nyumba za Jeshi la Polisi alimwagiza aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) kukomesha ukatili kwa raia na ukamataji raia usiozingatia taratibu zilizowekwa. Aidha, alikemea rushwa ili wananchi wapate huduma zinazostahili kutoka Jeshi la Polisi.

Katika hotuba yake ya uzinduzi wa Kamati ya kitaifa ya ushauri kuhusu utekelezaji wa mpango kazi wa ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa uliofanyika jijini Dodoma Desemba 16, 2021 Mheshimiwa Rais Samia alisema:

*"Niwapongeze kwa uamuzi wenu kwa kuweka ukomo wa kufanya upelelezi kufikia miezi sita, lakini mwaka mmoja kwa zile kesi kubwa, lakini bado tunaweza kufanya vizuri zaidi, kwa sasabu kucheleweshwa kwa upelelezi*

*kunaongeza mzigo kwa Serikali kuweka maabusu jela. Tukiangalia takwimu mpaka mwezi huu tarehe 22, idadi ya mahabusu katika jela zetu karibu sawa sawa na idadi ya wafungwa katika jela zetu, sasa."*

## 2.13 Heshima ya utu wa mtu

Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ni kiongozi anayependa kuona kila mtu anaheshimiwa, anathaminiwa na kutambuliwa utu wake; ndiyo maana katika kipindi cha uongozi wake amekuwa akikemea vikali vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji.

Katika hotuba yake akifungua kikao kazi cha Maafisa Wakuu wa makao makuu, na Makamanda wa mikoa na vikosi vya Jeshi la Polisi Agosti 25, 2021 Mheshimiwa Rais alitoa agizo hili kwa Jeshi la Polisi kukomesha unyanyasaji mitandaoni:

*"Lakini pia tukaangalie maendeleo ya utandawazi na TEHAMA na haki za watu wetu ndani ya nchi... Tunazungumza masuala ya unyanyasaji lakini wengi wananyanyaswa kupitia mitandao hii; anaye mnyanyasa kwa kujua anafanya makosa anatumia laini ambazo hata ukimtafuta TCRA humpati, hii katika haki za watu je kwenye usalama wa nchi, naomba Jeshi la Polisi mkajipange."*

## 2.14 Demokrasia

Mheshimiwa Rais amekuwa akihimiza demokrasia na

utawala wa haki. Ameruhusu vyama vyote kutekeleza majukumu yao ya kisiasa kwa kufuata sheria zilizowekwa. Mara baada ya kuapishwa aliunda kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kinachoongozwa na Prof. Rwekaza Mkandala. Alikutana na kikosi kazi hicho Machi 12, 2022na kupokea taarifa yake ambapo ameielekeza Wizara ya Katiba na Sheria kuandaa kanuni za uendeshaji wa vyama vya siasa.

Ameonyesha uvumilivu mkubwa wa kisiasa (political tolerance) kwa kukubali kufanya mazunguzo na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe siku moja baada ya kuachiwa huru na Mahakama Kuu ya Tanzania baada ya kukaa mahabusu kwa siku 216. Vilevile, amefanya mazungumzo na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa nchini kupitia kituo cha demokrasia Tanzania (TDC).

Mheshimiwa Rais pia alikutana na viongozi wa vyama vya siasa waliopo nje ya nchi. Alikutana na kuzungumza na Makamu Mwenyekiti wa chama kikuu cha upinzani, CHADEMA, Mheshimiwa Tundu Antipus Lisu akiwa ziarani nchini Ubeligiji. Matukio haya yameleta umoja na mshikamano na kumaliza utengano uliokuwa umejitokeza.

## 2.15 Ushiriki wa makundi maalum

i) Amedumisha haki ya kuabudu kwa raia wote

kulingana na imani zao;

ii) Amekutana na viongozi wa dini kwa lengo la kudumisha mashirikiano;

iii) Pia, amekuwa akipokea ushauri kutoka kwa viongozi wa dini wa kumtaka kudumisha amani na utawala wa sheria na haki za binadamu. Mapema mwaka Februari 22, 2022 alipokea ushauri kutoka kwa viongozi wa dini wa kutothubutu kujilinganisha na Mungu na yeye mwenyewe kueleza kuwa katika utawala wake hatakubali kulinganishwa na Mungu na atakuwa mnyenyekevu;

iv) Amekutana na makundi mengine kama ya wanafunzi, walemavu na wanawake na kusikiliza kero na mahitaji yao na kuhimiza kulindwa kwa haki zao.

## 2.16 Hifadhi ya haki za binadamu

Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anatambua nafasi na wajibu wa Asasi za Kiraia katika kutetea, kulinda na kukuza haki za binadamu nchini na hivyo amekuwa akizitia moyo wa kuendelea na majukumu yao kwa manufaa ya nchi na watu wake.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan imeweka mazingira wezeshi kwa

watetezi wa haki za binadamu kutekeleza majukumu yao, imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali katika kulinda na kukuza haki za binadamu na katika kusambaza elimu kwa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu.

Katika hotuba yake wakati wa Maadhimisho ya miaka 10 ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THDRC) jijini Dar es Salaam Mei 13 mwaka huu, Mheshimiwa Rais Samia alisema:

*"Serikali inayo nia ya dhati ya kuendelea kuchukua hatua za kisera, kisheria na kiutawala kutimiza malengo yote ambayo tumejiwekea yanayoendana na mwenendo wa haki za mwanadamu."*

Pia alisema kuwa:

*"Kazi ya kulinda haki ya mwanadamu tutaifanya sote ili kuwaletea wananchi maendeleo kwa sababu haki ya mwanadamu ni maendeleo, na maendeleo ni kutoa haki kwa wanadamu wanaokuzunguka."*

Vilevile aliongeza kuwa:

*"Serikali inayo kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba haki ya kila mmoja haiingiliwi na mwingine kama ilivyobainishwa kwenye ibara ya 29 na 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inawezekana kila mtu akatambua wajibu wake ndiyo maana nikasema wananchi wafundishwe, wasomeshwe, waelimishwe kujua haki na wajibu wao tutakapojua hilo hakuna atakayekwenda kumkwaza mwenziwe na atakapomkwaza mwenziwe atajua amevunja haki*

*ya mwenziwe, na kama amevunja haki ya mwenziwe sheria zipo kumshughulikia na hakutakuwa na manung'uniko...Kwa hiyo, niseme kwamba zile haki zilizobainishwa kwenye ibara ya 29 na 30 ya Katiba yetu ziende zikajulikane kwa wananchi."*

Hata hivyo, aliwaonya Watetezi wa haki za binadamu nchini kwa kuwaeleza kuwa:

*"Fanyeni harakati ya haki za binadamu kulingana na mazingira ya kitanzania."*

## 2.17 Utawala bora na uwajibikaji

Rais ameonesha kwa vitendo umuhimu wa kuzingatiwa kwa utawala bora nchini kwani misingi ya utawala bora inapokiukwa, haki za binadamu zinavunjwa. Yafuatayo ni baadhi ya yaliyofanyika:

**i)** Amedhihirisha uwazi katika matumizi ya fedha za Serikali. Kwa mfano mgawanyo wa fedha za mkopo za UVIKO 19 kwenye Halmashauri mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani ambapo kila mwananchi aliona mgawo huo kwa kila Halmashauri na kule Zanzibar;

**ii)** Alipoingia madarakani aliivunja Bodi ya Mamlaka ya Bandari nchini (TPA) kwa matumizi mabaya ya madaraka na kuiagiza Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa kufanya uchunguzi ili kuangalia vitendo vya kifisadi ikiwemo baadhi ya makampuni kulipwa fedha ya kutengeneza

mifumo lakini kazi hazikufanyika. Tuhuma hizi pia ziliibuliwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) katika taarifa yake ya Desemba 2021. Pia, Machi 28, 2021 alimsimamisha kazi Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari, Mhandisi Deusdedith Kakoko kwa matumizi mabaya ya madaraka;

**iii)** Februari 4 mwaka 2022 alimwagiza Waziri Mkuu kuunda Tume huru kuchunguza mauaji ya Mfanyabiashara wa madini huko Masasi, Mtwara aliyedaiwa kuuawa na Maofisa wa Polisi na kisha Jeshi la Polisi kuunda Tume ya kujichunguza, jambo ambalo Rais hakukubaliana nalo kwa kuwa ni kinyume na misingi ya utawala bora;

**iv)** Alitengua uteuzi wa aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Bwana Lengai Ole Sabaya kutokana na tuhuma ya matumizi mabaya ya madaraka yake;

**v)** Rais aliikemea Ofisi ya Rais TAMISEMI chini ya Waziri Suleiman Jaffo kwa wakati huo juu ya upotevu mkubwa wa fedha katika wizara hiyo;

**vi)** Alikemea rushwa ya ngono katika vyuo vikuu na vyuo vya kati nchini;

vii) Amesisitizia misingi ya haki katika utoaji wa huduma mbalimbali;

viii) Amekemea matumizi mabaya ya madaraka kwa watumishi wa umma;

ix) Amekemea ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa nguvu kwa kutumia "Task Force" ambazo huishia kwa wananchi kupoteza mali zao na kuumizwa licha ya Serikali kupata mapato;

x) Ameiagiza mamlaka ya mapato nchini (TRA) kukusanya kodi halali ya Serikali na kuitaka mamlaka hiyo kuacha tabia ya kuchukua mali za raia kwa nguvu, kuacha mara moja tabia ya kufunga biashara za wananchi na kuwataka wafanyabiashara kulipa kodi kwa mujibu wa sheria;

xi) Aliiagiza taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kushughulikia kwa haraka kesi zilizopo na zisilundikwe, kesi zisizo na mashiko zisipelekwe mahakamani, sheria za ushahidi ziangaliwe upya ili kulinda mashahidi;

xii) Ameruhusu kufunguliwa kwa akaunti za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kama vile Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDCs);

**xiii)** Amekubali Tanzania kuendelea kuwa mwanachama wa Mahakama ya Afrika na Watu (ACHPR) na kuruhusu wananchi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kupeleka malalamiko yao katika mahakama hiyo. Hatua hiyo ilipongezwa na Rais wa Mahakama hiyo alipomtembelea Ikulu Jijini Dar es Salaam Mei 27, 2021. Aidha, jumuiya za kimataifa zilipongeza juhudi hizo za Mkuu wa nchi kuendeleza mashirikiano na taasisi mbalimbali za kimataifa; na

**xiv)** Mara kwa mara amekuwa akisisitiza kuhusu uwazi na utawala wa sheria kama nukuu zifuatazo hapa chini zinavyoonesha:

*"Tunapoleta fedha Halmashauri hakuna siri tunataka wananchi waelewe, wajue kwamba fedha kiasi kadhaa zimekwenda kwenye eneo lao ili waweze kufuatilia utekelezaji."*

– Rais Samia Suluhu Hassan kwenye Mkutano wa hadhara uliofanyika Mei 19, 2022 uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora.

*"Niwapongeze kwa uamuzi wenu kwa kuweka ukomo wa kufanya upelelezi kufikia miezi sita, lakini mwaka mmoja kwa zile kesi kubwa, lakini bado tunaweza kufanya vizuri zaidi, kwa sasabu kucheleweshwa kwa upelelezi kunaongeza mzigo kwa Serikali*

*kuwaweka mahabusu jela tukiangalia takwimu mpaka mwezi huu tarehe 22, idadi ya mahabusu katika jela zetu karibu sawa sawa na idadi ya wafungwa katika jela zetu, sasa."*

– Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa Kamati ya kitaifa ya ushauri kuhusu utekelezaji wa mpango kazi wa ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa Desemba 16, 2021 jijini Dodoma.

## 2.18 Hitimisho

Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita na jinsi anavyoitaja Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania am waka 1977 Ibara ya 130 (1) (a-h) na Sheria ya Tume Sura 391 kifungu Na. 6(1) (a-o), Mheshimiwa Rais anaikumbusha Tume kutekeleza majukumu yake. Hii inamaanisha kuwa Mheshimiwa Rais anaitambua Tume, na kuonyesha utayari wa kuisaidia na kushirikiana nayo katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha, Tume inapoingia kazini itakuwa inatoa taswira na matakwa ya Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Ni wazi kuwa hatua zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais na Serikali yake zinahitaji wasimamizi (Oversight

institutions) ambapo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni miongoni mwao, kama inavyoelekezwa na Katiba.

Maoni ya Mheshimiwa Rais kuhusu haki za binadamu, hatua alizofikia katika kuzilinda, kuzikuza na kuziendeleza, inaipa Tume wajibu wa kuyasimamia. Aidha, matukio yanayoendelea kutokea yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukaji wa misingi ya utawala bora yanatakiwa kushughulikiwa na Tume mara moja pindi yanapotokea. Tume inaposimamia majukumu hayo itakuwa imeunga mkono juhudi za mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na Taifa ambalo haki za binadamu na misingi ya utawala bora inalindwa, inakuzwa, inahifadhiwa na kuendelezwa.

Hivyo, Tume ikiwezeshwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo itakuwa imemsaidia Mheshimiwa Rais na Serikali yake kufikia malengo yao katika kuwatumikia Watanzania wengi walio na shauku kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii yanayochochewa na uzingatiwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

***Mungu ibariki Tanzania,***
***Mungu ibariki Afrika,***
***Kazi iendelee!***

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
TANZANIA
COMMISSION FOR HUMAN RIGHTS
AND GOOD GOVERNANCE

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**
Mtaa wa Nyerere, Kitalu Na. 339, Kilimani
S.L.P 1049, DODOMA
Simu: +255 734 047 775; 734 119 978
Barua pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz